

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu: 2460117
Fax: 255 - 022 - 246011
e-mail: info@psc.go.tz;
Secretary@psc.go.tz;
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UBUNGO PLAZA,
BARABARA YA MOROGORO,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA WATAKIWA
KUWAJULISHA WATUMISHI MAHALI PA KUKATA RUFAA**

MWENYEKITI wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Jaji (mstaafu) Dkt. Steven James Bwana amewaagiza Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa umma kuhakikisha wanawajulisha watumishi wao wanaowachukulia hatua za nidhamu mahali pa kukata Rufaa pale wanapokuwa hawaridhiki na uamuzi uliotolewa dhidi yao.

Dkt. Bwana amesema hayo wakati wa kikao cha Tume kitakachofanyika kwa wiki mbili kilichoanza jana jijini Dar es Salaam. Amesema kutokana na kutokujulishwa na Mamlaka zao za Nidhamu muda uliowekwa kisheria wa kukata rufaa ndani ya siku 45 baada ya kupokea uamuzi, baadhi ya watumishi wa umma wamechukua muda mrefu kuwasilisha rufaa zao Tume ili kutafuta haki ambayo wakati mwingine wanaikosa kwa sababu tayari rufaa zao zinakuwa zimewasilishwa nje ya muda uliowekwa kisheria.

"Mamlaka za Nidhamu hakikisheni warufani wanaandikiwa barua ya uamuzi inayomuelekeza wapi anatakiwa kukata rufaa yake, ambapo ni Tume ya Utumishi wa Umma, na kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 muda uliowekwa ni ndani ya siku 45. Mamlaka za Nidhamu tambueni kuwa moja ya haki ambazo mtumishi wa umma anatakiwa kupewa ni kusikilizwa. Wakijulishwa ipasavyo itasaidia kuondoa watumishi wasiokuwa na

hatia kuona wameonewa na itasaidia pia kwa waliofanya makosa kuchukua hatua stahiki” amesema.

Kwa upande wa watumishi wa umma, Mheshimiwa Dkt. Bwana amesema kuwa watumishi wa umma wanapaswa kufahamu vizuri Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayotolewa pamoja na Maelekezo halali ya Viongozi wa Serikali, kwani kutokujua Sheria haizuii kuchukuliwa hatua stahiki pale mtumishi anapofanya makosa.

Aidha, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, bwana Nyakimura Muhoji amewajulisha Makamishna wa Tume kuwa hivi sasa Sekretarieti ya Tume inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Muundo mpya. Hivyo, rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma yanayowasilishwa Tume yanashughulikiwa katika Idara moja. Bwana Muhoji, amewataka Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuwasilisha Tume vielelezo vyote muhimu kwa wakati ili haki iweze kutendeka kati ya Mrufani na Mrufaniwa.

Mkutano huu wa Tume unafanyika ambapo rufaa na malalamiko mbalimbali ya watumishi wa umma wanaopinga uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Ajira na Mamlaka za Nidhamu. Vile vile Taarifa mbalimbali zinazohusu uendeshaiji wa masuala ya Rasilimali watu katika Taasisi za Umma zitawasilishwa.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
05 Novemba, 2019